

HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTIAJI SAINI WA MIKATABA YA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU KATIKA JIJI LA DAR ES SALAAM(DMDP) KATIKA MANISPAA YA KINONDONI LEO JUMAMOSI TAREHE,2 JUNE,2018.

Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni leo jumamosi tarehe 2,June,2018 imesaini mikataba ya miradi ya uboreshaji wa Miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam {DMDP}fungu la5 na 6 na Makampuni mawili yaliyoshinda Tender ya Kimataifa yenye thamani ya **Tshs 39,087,977,826** kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, Mifereji,taa za barabarani,njia za watembea kwa miguu,soko,na vyoo vya umma katika kata tatu za Tandale,na Mwananyamala Manispaa ya Kinondoni na Kata ya Mburahati katika Manispaa ya Ubungo.


Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni Ndugu Aron T. Kagurumjuli amesema, wakati akitoa ufafanuzi wakati wa utiaji saini kuwa , Kampuni ya CRJE(EAST AFRICA LTD) imepewa kazi ya fungu la 5 (package5)katika kata za Tandale na Mburahati kwa ajili miradi ya ujenzi wa barabara Km 7.96 kwa kiwango cha lami, mifereji, taa za barabarani, njia za watembea kwa miguu na vyoo vya umma kwa thamani ya **Tshs ,20,340,139,282.84** inayotarajia kuanza tarehe 4June 2018 na kukamilika tarehe 3,Septemba 2018.

Aidha ameitaja Kampuni ya CHINA RAILWAY SEVENTH GROUP CO.LMT kupewa kazi ya fungu la 6(package 6) kwa miradi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Km.6.30,mifereji,taa za barabarani, njia za watembea kwa miguu, soko na vyoo vya umma katika Kata ya Mwananyamala yenye thamani ya **Tshs,18,737,838,543.84** inayotarajia kuanza tarehe 4,June, 2018 na kukamilika tarehe 3 Septemba 2018 na kwamba miradi yote inahusisha fidia ya **Tshs 2,001,054,325.49** kwa wafidiwa 184.

Akizungumza Katika hafla ya utiaji saina Mikataba hiyo Mstahiki meya wa Manispaa ya Kinondoni Mhe. Benjamin Kawe Sitta alimshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr John Pombe Magufuli na Serikali kuu kwa Ujumla kwa jitihada zinazofanywa kuboresha miundombinu kwa wakazi wanaoishi katika maeneo duni na kuwataka wakandarasi waliopewa kazi hiyo kukamilisha kwa wakati na kuzingatia masharti yote.

Mwisho, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni Mhe. Ally Hapi aliyeshuhudia utiaji saina wa miradi hiyo, pamoja na kupongeza juhudi za serikali kwa kazi kubwa inayofanya aliwataka wakandarasi wanaopewa miradi hii mikubwa na Serikali kutekeza kwa ufanisi na kuzingatia thamani ya fedha yaani **Value of money**. Aidha aliwaomba kuangalia uwezekano wa kuzisaidia jamii zilizopo katika maeneo husika kama mchango wao kwa jamii hizo yaani **corporate Social responsibility**.

Imetolewa na :-



Sebastian M. Mhowera

**AFISA UHUSIANO WA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINONDONI.**